Stockholms stad

# Digital vardag

Kuhusu utumiaji/uwekaji wa kidijitali-kwa ajili yako wewe ambaye ni mhamiaji mpya na unaishi katika mji wa Stockholm.



Nchini Sweden/Uswidi, sehemu nyingi katika jamii zinawekwa kidijitali.
Katika brosha/kipeperushi hiki unaweza kusoma kuhusu maana yake ni nini na jinsi unavyoweza kuwa kidijitali zaidi. Ni muhimu kuweza kutumia zana/vifaa vya kidijitali ili kushiriki katika kupokea huduma mbalimbali kwenye jamii.

# Utumiaji/Uwekaji wa kidijitali

**Utumiaji/uwekaji wa kidijitali ni nini?**
Utumiaji/uwekaji wa kidijitali ina maana kwamba tunatumia teknolojia ili kukifanya kitu kiwe bora na rahisi.
Tunaokoa muda na pesa tunaposhughulikia masuala yetu ya kikazi kwa njia ya kidijitali.
Kwa mfano, siku hizi tunatuma e-post yaani barua-pepe badala ya barua ya kawaida.
Kuna faida nyingi na utumaji kwa njia ya barua-pepe.



**Barua:**

- inagharimu pesa kutuma
- inachukua muda:
- mtu anapaswa kwenda posta ili kutuma barua hiyo
- inachukua siku kadhaa hadi Tarishi awasilishe barua.


**Barua-pepe/e-post:**

- bure, haigharimu chochote
- inawasilishwa ndani ya nukta/sekunde kadhaa

# Mamlaka za kidijitali

Mamlaka zote nchini Sweden zina tovuti yaani webbsida. Kwenye ukurasa wa wavuti utapata taarifa sahihi na za kisasa. Kila wakati tumia tovuti za Serikali kama chanzo chako cha habari yaani taarifa.

Pia unaweza kuwasiliana na Mamlaka kidijitali, bila ya ulazimu wa kuondoka nyumbani kwako. Unaweza kutuma barua-pepe, kutumia chatti yaani gumzo au kupiga simu. Maelezo ya mawasiliano yanapatikana kila wakati kwenye ukurasa wa wavuti. Huko vilevile utapata anwani ya Ofisi iliyo karibu nawe, endapo unahitaji kuitembelea.




Jaribu kutembelea baadhi ya kurasa za wavuti!

**www.arbetsformedlingen.se**
**www.forsakringskassan.se**
**www.migrationsverket.se**
**www.stockholm.se**

# Utafiti/fanya utafiti/tafuta taarifa

Unaweza kuzipata taarifa/tafiti karibu zote kuhusu swali lolote kwenye mtandao.
Unatafuta kwenye mtandao kwa kutumia injini ya utafutaji.
Kwa mfano Google. Fungua kivinjari yaani browser/mushakisha kwenye simu yako ya mobil:

Kwenye **iPhone**: Safari

Kwenye **Android**: Google Chrome

Jaribu kutafuta jibu la swali!





Andika swali lako kwenye kisanduku cha kutafutia.
Kwa mfano:

- Hali ya hewa itakuwaje kesho?
- Anwani ya ofisi ya Wakala wa Kodi na Ushuru
- Nambari ya simu ya shule yako ya SFI

# Ni programu maalum zilizopo mtandaoni ziitwazo appar

Appar ni programu ambazo unazipakua kwenye mobil yako,
Kuna aina nyingi tofauti za hizo programu/appar, kwa mfano
programu ya gumzo/chatt, michezo na programu ambapo
unaweza kuangalia video au kusikiliza muziki.
Unazipakua progamu hizo kutoka kwenye App Store (iPhone)
au Google Play (Android).




# Barua-pepe yaani E-post




Kutuma barua-pepe, au ”barua-pepe” ni kutuma ujumbe kwa njia ya kidijitali.
Ni bure yaani bila malipo kutuma barua-pepe.
Barua-pepe hutumwa kwa mara moja yaani muda huohuo na baada ya nukta/sekunde humfikia mhusika yule mpokeaji.
Unaweza kuunda/kutengeneza barua-pepe yako bila malipo yaani bure kutoka kwenye huduma mbalimbali za barua-pepe, kwa mfano Gmail.
Ili kuunda anwani ya gmail, nenda kwenye tovuti **www.gmail.com**.

# BankID




Pasipoti yako au leseni ya udereva ni kitambulisho na inakutambulisha kama wewe ndiye mhusika.
BankID ni kitambulisho cha kidijitali.
BankID inakutambulisha kwamba wewe ndiye mhusika kwenye mtandao.
BankID hufanya kazi kama ufunguo ambapo unajitambulisha kwenye huduma mbalimbali za mtandaoni.
Unapata BankID kutoka kwenye Benki yako.

# Benki ya mtandao

Badala ya kwenda katika ofisi za benki, unaweza kushughulikia masuala yako ya benki kidijitali.
Wakati unapofungua akaunti ya benki unapata uwezo wa ufikiwaji wa/kuifikia benki ya mtandao ambayo inakuwa wazi masaa yote yaani usiku na mchana.
Unaweza kulipa bili na kuhamisha pesa bila uhitaji wa kuondoka nyumbani kwako.

# Misimbo/Nambari ya QR yaani Kode ya QR

Misimbo/Nambari ya QR ni kama msimbo-pau/kode y`akabari
na unakupeleka kwenye ukurasa wa wavuti.
Ili kutumia msimbo/nambari ya QR:

1. Fungua kamera kwenye simu yako ya mobil.
2. Elekeza kamera kwenye Msimbo wa QR.
3. Kiungo yaani lenki kupitia Msimbo wa QR kitaonekana. Bonyeza kwa maana nyingine ikimaanisha iminye/iguse ili kufikia ukurasa wa wavuti

**Jaribu kuchanganua yaani kuscanni msimbo/nambari!**

# Tiba kwa njia ya kidijitali

Endapo una maswali kuhusu afya yako, unaweza kupatiwa usaidizi kidijitali. Unaepukaana na ulazimu wa kutakiwa kutembelea zahanati/hosipitali ndogo ikimaanishwa vårdcentralna na kusubiri kwenye msitari. Kwenye 1177.se unazipata taarifa/habari nyingi nzuri pamoja na wapi unakoweza kuelekea unapohitaji huduma ya matibabu. Pia unaweza kupiga 1177 na kuzungumza na muuguzi/nesi.

Changanua msimbo wa QR ili usome zaidi katika lugha tofauti!

# Usalama kwenye mtandao

Mtandao ni sehemu kubwa /pana yenye uwezekano mwingi. Unaweza kupata majibu ya maswali yako, kujifunza mambo mapya, kupata marafiki wapya.
Mtandao pia una upande mdogo wa aina yake.
Kama ilivyo katika Ulimwengu wa kweli, unaweza kukutana na watu wanaoeneza habari/taarifa za uwongo na kutaka kukudanganya.
Ni muhimu kuwa mwangalifu wakati unapotumia mtandao na kwamba unalinda taarifa zako za faragha ikimanishwa za siri.



**Usishirikishe wengine kuhusu taarifa zako za binafsi zenye maelezo ya namna ya kuingia, nenosiri/pasiwedi au misimbo/nambari.**
Unaweza kukutana na watu ambao wanataka uwapatie taarifa zako binafsi, data zako yaani habari au kuhusu pesa katika akaunti yako ya Benki.
Haya ni mambo ambayo ni yako binafsi, kamwe usishirikishe watu wengine.



**Kuwa makini kwenye kufahamu ujumbe na viungo/lenki vya kutiliwa shaka.**
Wakati mwingine walaghai hujaribu kuwadanganya wengine kwa kutuma jumbe ghushi/bandia. Hizo jumbe/taarifa huonekana kama zinatoka benki au wakala wa Serikali. Endapo huna uhakika mtumaji ni nani, usifungue lenki/viungo vya kutiliwa shaka.



**Pata habari/taarifa kutoka kwenye vyanzo vinavyoaminika.**
Kwa bahati mbaya, kuna habari za uwongo zinazoenezwa kwenye mtandao na ni muhimu kudhibiti yaani uangalie kwa makini vyanzo vyake kwa maana vya habari. Kwa mfano, ikiwa unatafuta majibu ya posho yenye usaidizi kuwahusu watoto-tembelea tovuti ya Wakala wa Bima ya Kijamii ya Uswidi, ambayo husasishwa kila mara na taarifa za sasa ikimaanishwa kuwa zihusikazo muda huu uliopo.

# Kamusi

svenska-engelska

| | |
|---|---|
| ansluta | unganisha |
| användarnamn | jina la mtumiaji |
| app | programu |
| avbryt | ghairi/acha |
| avsändare | mtumaji |
| batteri | betri |
| bifoga fil | faili lililoambatishwa |
| bild | picha |
| brevlåda | sanduku la barua |
| chatt | gumzo/piga soga |
| datormus | panya ya kompyuta |
| dela | shirikisha |

| | |
|---|---|
| e-post | barua-pepe/e-post |
| e-tjänst | huduma ya kielektroniki |
| felmeddelande | ujumbe wa makosa |
| fil | faili |
| fönster | dirisha |
| hemsida | tovuti |
| inkorg | kikasha/inboksi |
| installera | sakinisha/ingiza/funga |
| inställningar | mipangilio |
| klistra in | kubandika/kuweka |
| kontakter | mawasiliano |
| kopiera | nakili |
| ladda ner | pakua |
| laddare | chaja |
| logga in | ingia mtandaoni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| logga ut | toka mtandaoni | skrivare | printa |
| länk | kiungo/lenki | skrivbord | dawati/meza ya kuandikia |
| lösenord | nenosiri/pasiwedi | skräp | takataka/ uchafu |
| mapp | folda- | skärm | skrini |
| meddelande | ujumbe | språk | lugha |
| meny | yaliyomo | svara | jibu |
| min sida | ukurasa wangu | svara alla | jibu yote |
| mottagare | mpokeaji | sök | tafuta |
| notis | taarifa | sökmotor | injini ya utafutaji |
| nätverk | mtandao | tangentbord | kibodi |
| papperskorg | kikapu cha taka | uppdatering | sasisha-kuifanya ya sasa hivi |
| program | programu | utkast | kutupwa nje |
| radera | kufuta | vidarebefordra | endelea kupele ka kwingine huko mbele |
| ringa | wito/kupiga simu | webbläsare | Kivinjari-yaani browser/musha-kisha |
| skickat | imetumwa | webbsida | ukurasa wa wavuti |

# Jipatie/jifunze maelezo zaidi kuhusu zana za/vifaa vya kidijitali.

Kuwa na uwezo wa kutumia zana za kidijitali ni muhimu sana.
Unaweza kujifundisha mwenyewe au kuchukua kozi.
Changanua/scanna msimbo wa QR ili kusoma zaidi.

Kwenye tovuti utapata taarifa zaidi kuhusu mahali pa kuelekea ili kujua mambo yahusikayo kwa makusudi ya kijifunza zaidi.

Kila la kheri!
Bahati njema!

# Msaada wa kidijitali

Je, unahitaji usaidizi kwenye kutumia zana za/vifaa vya kidijitali? Kuna maeneo kadhaa ambapo unaweza kurejea ili kujua.

## Welcome House

Katika **Welcome House** unaweza kusoma kozi moja kuhusu zana za kidijitali au unapatiwa usaidizi na maswali yako ya kidijitali.




Welcome House iko katika **Medborgarplatsen 25**.

Changanua/scanna msimbo QR ili kutembelea tov-uti ya Welcome House na kuona saa za ufunguzi za sasa/masaa wazi.

## Maktaba

Kwenye Maktaba unaweza kuazi-ma kompyuta na kupata usaidizi wa kuitumia.

Pata Maktaba ya karibu:

## Ofisi ya Wananchi/Raia

Pata ofisi ya Wanan-chi/Raia ya karibu.

Kwenye ofisi ya Wananchi zinakuwepo kompyuta ambazo unaweza kuazima na kupata usaidizi wa jinsi ya kuzitumia.

## Statens Servicecenter

Katika ofisi za huduma unaweza kupata usaidizi wa huduma za kielektroniki na masuala ya kidijitali katika Wakala wa Uajiri, Hazina ya bima ya Uswi-di, Wakala wa Uhamiaji, Mamlaka ya Pensheni, na Wakala wa Ushuru wa Uswidi.

Changanua/scanna msimbo QR na utafute ofisi ya huduma iliyo karibu nawe.